## HUDUMA YA TUJENGE NYUMBA YA MUNGU

### Historia ya Huduma ya Tujenge Nyumba ya Mungu

Huduma hii ilianza wakati ambapo mimi mwalimu Mbogo Kerenge ambaye pia ni mwandishi wa kitabu cha *Nguvu Iliyopo Katika Sadaka Isiyo ya Kawaida*, nilipokuwa katika huduma ya kufundisha neno la Mungu Vijijini huko mkoani Mara. Nilialikwa kushiriki katika ibada ya siku ya Jumapili katika Kijiji cha Kurusanga Wilayani Bunda Mkoani Mara. Nilipofika mahali hapo nikiwa na mke wangu na mtoto wangu Jayden tarehe 6 Septemba 2020**,** nilikuta watu wakimwabudu Mungu katika mazingira duni sana.

